SHULE: ……

JINA: …….. NAMBARI: …….. DARASA……

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2

LUGHA

JULAI 2018

KIDATO CHA NNE

MUDA: SAA 2½

MAAGIZO

(a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(b) Jibu maswali yote.
(c) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
(d) Majibu yote LAZIMA yaandikwe kwenye kijitabu hiki cha maswali.
(e) Karatasi hii ina kurasa tisa zilizopigwa chapa.
(f) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na maswali yote yamo.

Kwa matumizi ya mtahini pekee.

		A
A		

1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Kweli, taarifa zimeonekana katika vyombo vya habari kuwa vijana wetu wanajua mengi kutushinda. Wengi wameshiriki ngono ilhali tukiwa nyumbani sisi wazazi tunawaona malaika.

Kwa kweli taarifa hizo ni sawa na mbiu ya mgambo kuwa tuzungumze na watoto wetu kuhusu suala hili. Ni vyema wajue kutoka kwetu kuliko kufahamu kutoka kwa wengine ambao badala ya kuwaelekeza wanawapotosha. Mara nyingi wakiwa katikati ya marika, wao hushinikizana kujaribu na wengi wanaamini kuwa kufanya mara moja sio tatizo. Lakini kile ambacho hawaelewi ni kuwa hiyo mara moja inaweza kuwabebesha mimba ama kuwaambukiza ukimwi na maradhi ya zinaa. Aidha, utu huumbuliwa na hivyo kupotoka kimaadili. Hayo ni masuala ambayo wazazi hawafai kuyaonea haya tena kwa sababu watoto wetu wanayafahamu lakini cha msingi ni kujua ukweli na hatari zilizopo.

Wazazi wengi wamewatelekeza watoto wao. Wengi husema kuwa wanawatimizia kila hitaji. Hii inamaanisha kuwa unalipa karo kwa wakati unaofaa, kuna chakula cha kutosha nyumbani, mavazi wako nayo na pia pesa za mfukoni wanazo. Lakini kile ambacho hawana ni muda wa kuwa na watoto wao. Baadhi ya matatizo tunayokumbana nayo yanaweza kutatuliwa ikiwa wazazi watatenga muda wa kuzungumza ana kwa ana na watoto wao.

Ni kweli wengi wamesingizia kazi kwa sababu wanaamka mapema na kurudi usiku. Lakini hiyo kazi ina maana gani ikiwa kesho utajipata na mjukuu wa kulea bila kutarajia? Kwa hivyo, wazazi lazima waache kuwaachia wafanyikazi wa nyumbai jukumu lao ama kuwapeleka katika shule za bweni mapema kwa sababu wanawaona kuwa mzigo. Pia kuna wale ambao huwachwa hata vilabuni kwa madai kuwa wanakutana tu na marafiki zao.

Baadhi ya mavazi, ingawaje huwafanya watoto wao kuonekana kama wanaoenda na wakati ama ya kisasa, huwa hayafai. Lazima wafunzwe tangu wakiwa wachanga kuhusu suala la kujiheshimu. Haifai kufikiria kwamba kwa sababu ni mtoto anaweza kuvaa chochote kile. Mtoto anafaa kuvishwa mavazi ya heshima. Pia, wazazi wachunge mavazi yao wenyewe.

Maswali

a. Eleza dhamira ya mwandishi wa makala haya. (alama 2)

……

……..

b. Kushiriki ngono mapema kwa vijana kuna athari gani kulingana na makala haya? (Alama 4)

……
……
……
……

c. Wazazi wamechangia vipi shida zinazokumba vijana chipukizi? (Alama 4)

……
……
……
……..

d. Taja majukumu manne makuu ya wazazi kulingana na makala haya. (Alama 4)

……
……
……
……

e. Eleza maana ya maneno haya kimuktadha.
   a) Madai (alama 1) ……
   b) Mbiu ya mgambo (alama 1) ……..

2. UFUPISHO

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Katika kipindi cha mwongo mmoja uliopita, tumeshuhudia mabadiliko na maendeleo makubwa kuhusu vyombo vya habari nchini Kenya. Hapo awali, redio ndicho chombo cha habari cha kipekee kilichotamalaki kote nchini. Familia nyingi ziliweza kumiliki chombo hiki. Runinga ilikua miliki ya wachache, hasa mabwenyenye. Sasa hivi hata akina yahe nchini na mashambani wanamiliki chombo hiki.

Runinga kama kifaa kingine chochote cha mawasiliano kina manufaa yake. Kwanza kabisa ni nyenzo mwafaka ya kufundisha. Vipindi vinavyopeperushwa katika runinga huwa na mafunzo kemkem kwa mtu wa kila rika. Hali kadhalika, runinga huweza kuleta vipindi ambavyo huwafahamisha watu mambo yanayoendelea katika mazingira yao na duniani. Aidha, runinga ikitumika pamoja na michezo ya video, hasa ya kielimu, huwafanya watu kujenga umakini pamoja na kuchua misuli ya ubongo na kuwafanya watu kuwa macho wanapofanya kazi.

Fauka ya hayo, televisheni ni chemichemi bora ya kutumbuiza na kuchangamsha. Hakuna mtu asiyependa kuchangamshwa na kuburudishwa. Televisheni ni mojawapo ya vyombo mwafaka vya kutekeleza hayo kutokana na vipindi vyake. Uburudishaji huu huwa ni liwazo kutokana na shinikizo na migogoro tunayokabiliana nayo kila siku. Uburudishaji huu hupatikana kwa urahisi majumbani mwetu.

Vivyo hivyo, runinga hutumika kama nyenzo ya kuendeleza utamaduni, kaida na amali za jamii. Vingi vya vipindi vya runinga huwa ni kioo ambacho huakisi mikakati na amali za jamii.

Kwa upande mwingine, hakuna kizuri kisichokuwa na dosari. Licha ya manufaa yake, televisheni imedhihirika kuwa na udhaifu wake. Kwanza, baadhi ya vipindi vya runinga na video hujumuisha ujumbe usio na maadili, kama vile – matumizi ya mabavu, ngono za kiholela, lugha isiyo na adabu, ubaya wa kimavazi na maonevu ya rangi, dini, jinsia, kabila na utamaduni. Si ajabu kuwa baadhi ya vijana wetu wanaiga baadhi ya mambo haya. Vijana wetu siku hizi wameingilia ulevi wa pombe na afyuni, ngono za mapema kabla ya ndoa na mavazi yanayowaacha takribani uchi wa mnyama. Wengi wamekopa na kuyaiga haya kutoka katika runinga. Ukiwauliza wafanyacho, watakujibu kuwa ni ustaarabu kwani wameupata katika runinga.

Matumizi ya runinga na michezo ya video yasiyodhibitiwa, huweza kuwa kikwazo cha mawasiliano bora miongoni mwa familia. Matumizi kama haya huwapa wanafamillia fursa ya kujitenga. Imedhihirika kuwa runinga haichangii kujenga uhusiano bora wa kijamii. Ukilinganisha na vyombo vingine vya burudani ambavyo hutoa nafasi ya watu kutangamana na kujenga uhusiano bora, televisheni haichangii haya. Badala yake tajriba ya televisheni huwa ya kibinafsi. Hali hii inapotokea katika kiwango cha familia televisheni inaweza kutenganisha wazazi na watoto wao.

Halikadhalika, runinga na video aghalabu hueneza maadili yasiyofaa. Mathalani baadhi ya vipindi vya televisheni huendeleza hulka ya kuhadaa, ngono za kiholela, kuvunjika kwa ndoa,n.k. hulka hizi zisizoendeleza maadili ya kijamii huchukuliwa kama zinazofaa na zinafuatwa na waliostaraabika. Huu ni upotovu.

Isitoshe, baadhi ya matangazo huhimiza matumizi ya madawa ya kulevya kama tembo na sigara. Vitu hivi vinapotangazwa, hupambwa kwa kila hali na udanganyifu mwingi ambao huwavutia vijana na watoto wengi. Si ajabu mtu anapowauliza wanaotumia vileo hivi walivyoanza, watajibu kutokana na athari na matangazo katika runinga na vyombo vingine.

Utafiti umeonyesha kuwa vipindi vya runinga na video ni chanzo cha matumizi ya nguvu za mabavu miongoni mwa wanafunzi. Wazazi wengi huchukulia vibonzo katika televisheni kuwa vinalenga kuburudisha tu na havina ubaya wowote. Lakini ukweli ni kuwa, vipindi vingi vya vibonzo hushirikisha matumizi ya hila na nguvu za mabavu. Haya huibusha hamu ya vijana na watoto huyaiga.

Kwa hivyo, ni muhimu wazazi na jamii kutambua madhara ya televisheni. Utambuzi huu utawafanya wawaelekeze vijana na watoto jinsi ya kutumia televisheni na video ili kuepukana na madhara yake.

Maswali

(a) Kwa kuzingatia habari uliyosoma eleza manufaa ya runinga kama chombo cha mawasiliano. (maneno 50-60)alama 5

MATAYARISHO

……
……
……
……
……
……
……

JIBU

……
……
……
……
……
……
……

(b) Kwa maneno kati ya 60-70, fupisha taarifa hii kuanzia aya ya tano hadi mwisho. (alama 8)

MATAYARISHO

……
……
……
……
……
……
……

JIBU

……
……
……
……
……
……
……
……

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) Silabi ni nini? (alama 2)

……
……

(b) Andika kinyume cha:

Msichana aliingia darasani kwa haraka. (alama 2)

……

(c) Tambua viambishi awali na tamati katika kitenzi:

Aliyemlia (alama 2)

……
……

(d) Akifisha:

sikiliza bwana mdogo siku hizi tunaishi katika jamii ambayo imebadilika hayo mawazo yako ya zama kongwe hayatakufikisha popote alifoka abdi (alama 3)

……
……
……
……

(e) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia matawi. (alama 4)

Wote warefu ni wanafunzi.

……
……
……
……
……

(f) Onyesha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi hii:

Nyumba iliyojengwa jana imebomolewa. (alama 2)

……
……

(g) Tunga sentensi sahihi ukitumia vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizoko kwenye mabano.

(i) –fa(fanyia) (alama 1)

……

(ii) soma (tendesheana) (alama 1)

……

(h) Ainisha vielezi katika sentensi ifuatayo:

Juma alitukumbusha alivyotutembelea mara kadha mwaka jana. (alama 2)

……
……

(i)Onyesha aina ya shamirisho katika sentensi:

Mzazi alimbebea mtoto vitabu kwa mkoba. (alama 3)

……
……

(j) Tambua aina ya vitenzi katika sentensi:

Amekuwa akilala kwa vile yu mgonjwa. (alama 3)

……
……
……

(k) Taja na utofautishe vipasuo vya ufizi. . (alama 2)

(i) ……

(ii) ……

(l) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kutumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari.

Amegura mjini kwa sababu ya **mvulana** huyo. . (alama 3)

……

(m) Yakinisha:

Hajanivunjia mlango wala kuniibia. (alama 2)

……

(n) Onyesha aina za nomino katika sentensi ifuatayo na utambue zimo katika ngeli gani.

Kamati iliushuku werevu wake. (alama 2)

……

(o) Toa maana mbili za sentensi:

Alisimamisha gari njiani. (alama 2)

……
……

(p) Eleza matumizi ya “na” katika sentensi:

Njambi na Halima wanaandaliwa chakula na Hamedi. (alama 3)

……
……

(q) Tumia mzizi “enye” katika sentensi kama kiwakilishi. (alama 1)

……

4. ISIMU JAMII

(a) Eleza sababu TANO zinazowafanya watu kuchanganya msimbo. (alama 5)

……
……
……
……
……
……
……

(b) Kwa kutolea mifano mwafaka eleza sifa TANO bainifu za sajili ya maabadini. (alama 5)

……
……
……
……
……
……
……
……
……